Serikali inapanga Kufanya nini kwenye Elimu?

Ahadi za Serikali 2014/2015

Utangulizi

Kupitia mikutano ya kila mwaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, serikali imekuwa ikitoa ahadi mbalimbali kupitia mawaziri na manaibu mawaziri kutokana na maswali mbalimbali yanayoulizwa na wabunge. Ahadi na maagizo haya yanayotolewa na viongozi hupaswa kufuatiliwa na wananchi ili kuhakikisha kuwa serikali inawajibika kikamilifu kwa wananchi wake kwa kuzitekeleza ahadi hizo. Uwajibikaji wa viongozi hupimwa kwa namna wanavyotekeleza ahadi walizotoa kwa wananchi hususani zile zinazogusa maisha yao ya kila siku.

Kwa kuzingatia umuhimu huu shirika la HakiElimu limekuwa likifuatilia kila mwaka ahadi mbalimbali za serikali katika sekta ya elimu na kuzichapisha kwa lengo la kuikumbusha serikali kutimiza ahadi zake. Ahadi hizi huwawezesha wananchi kufuatilia utekelezaji wake na hivyo kuimarisha dhana ya utawala bora unaowajibika kwa upande wa serikali kwa kutimiza ahadi zake. Chapisho hili ni mkusanyiko wa ahadi zilizotolewa Bungeni mwishoni mwa mwaka 2013 na katika Bunge la bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mwananchi anawezaje kufuatilia ahadi za serikali katika elimu?

- Kwa kushiriki katika vikao vya kijiji, mtaa au kata nakutumia fursa hiyo kuhoji utekelezaji wa ahadi za serikali katika elimu.
- Kutafuta na kusoma ripoti mbalimbali za serikali kama MMEM ,MMES, Bajeti ya Elimu na kujenga hoja kuhusu ahadi zilizotolewa na kuwasiliana na mbunge wake ambaye ana jukumu la kufuatilia ufumbuzi wake serikalini.
- Kujenga hoja ya ufuatiliaji wa ahadi za serikali na kuifikisha katika halamashauri kwenye kitengo cha elimu au asasi zinazojishughulisha na elimu kama HakiElimu kwa hatua zaidi za ufuatiliaji serikalini.

Je, Unazifahamu Ahadi za Serikali katika Mwaka 2014/2015?

Elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu

Kwa mujibu wa taarifa za Bunge ahadi ifuatayo ilitolewa na Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mh.Jestina Mhagama(28 Mei, 2014). Akijibu swali la Mh. Susana .A. Lyimo kuhusu shule zinazojengwa sasa hivi kuwa bado hazizingatii mazingira rafiki kwa watoto wenye ulemavu:-Alisema, mpango wa ujenzi katika elimu ya Sekondari yaani MMES II kwa sasa hivi kipaumbele kimewekwa na maagizo makali yametolewa kwamba kila jengo litakalojengwa lazima lizingatie mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu.

Elimu kwa mtoto wa kike

Kwa mujibu wa taarifa za Bunge ahadi zifuatazo zilitolewa na manaibu mawaziri wa Wizara za Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

- Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto Mh. Sophia Simba (28 Mei, 2014) akijibu swali la Mh. Christowaja .G. Mtinda lililokua likiuliza je? Tanzania inatoa taarifa gani juu ya kipengele kinachotaka kuwepo mipango thabiti itakayosaidia wasichana kuendelea na masomo, ikiwa ni pamoja na wale wanaokatiza masomo kutokana sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito usiotegemewa? Alisema mkakati uliopo kwa hivi sasa ni pamoja na kujenga mabweni ya wasichana katika shule za sekondari za kata pia umuhimu wa kuwaelimisha wanafunzi wa kike na wakiume kuhusu elimu ya uzazi ili kuepukana na tatizo hili.

Jedwali la 4: Idadi ya wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari wanaoacha shule kwa sababu ya ujauzito

Jumla	Jumla
2009	1768
2010	1056
2012	2433

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

- Serikali imeahidi kuwepo na mkakati kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kuwepo na ushirikiano na Wizara ya Elimu kuwa

kwa wale wanafunzi wa kike wadogo watakaopata ujauzito ambao utapelekea wao kukatiza masomo yao kupata elimu ya MEMKWA. Na pia mikakati mengine ni kuwaweka wanafunzi hawa karibu na shule zao ili kusiwe na urefu wa kutembea wakati wanakwenda shule.

- Naibu waziri wa elimu na mafunzo ya Ufundi Mh. Jestina Mhagama(30 Mei, 2014) aliahidi pia kwa kusema serikali imejipanga kuinua Elimu ya msingi kwa kuanzisha program mbalimbali ambazo zitawafanya watoto wa kiume na wa kike wajue stadi za kujua kusoma, kuandika, na kuhesabu. Serikali imetenga bajeti ya kutosha na serikali imejipanga vizuri pamoja na miradi mingine mingi.

Ukaguzi wa shule

Kwa mujibu wa taarifa za kumbukumbu za Bunge ahadi zifuatazo zilitolewa Bungeni kuhusiana na Idara ya ukaguzi.

- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mh. Jenister Mhagama (20 Mei, 2014) akijibu swali lililoulizwa na Mh. Dustan D. Mkapa mbunge wa Nanyumbu, aliyeuliza ni lini serikali itaipatia gari idara ya ukaguzi wa elimu wilaya ya Nanyumbu. Mh. Mhagama alisema; serikali imekamilisha mpango wa ununuzi wa magari 36 kupitia mpango wa Global Partnership for education (GPE), yatakayonunuliwa katika mwaka wa fedha 2014/15, na hivyo kufanya magari yatakayonunuliwa kufikia 45, yakiwemo 9 yaliyonunuliwa mwaka 2013/14. Magari haya yatasambazwa katika wilaya husika. Mh. Jenister Mhagama alimfahamisha Mh. Dustan Mkapa kuwa wilaya yake ya Nanyumbu tayari imeshapatiwa gari la ukaguzi wa shule lenye namba za usajili STK 7160 Toyota Hilux Double Cabin.

- Naibu waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za mikoa na serikali za mitaa (Elimu), Mh. Kassim Majaliwa (19 Mei, 2014) akijibu swali la Mh. Salome Mwambu mbunge wa Iramba mashariki, ambaye aliwasilisha hoja yake kuelezea wilaya mpya ya Mkarama ambayo haina gari wala ofisi ya ukaguzi. Mh. Majaliwa aliahidi kuwa wizara yake kwa kuanzia inawasiliana na ofisi ya TAMISEMI ili waanze kuisaidia wilaya hiyo ipate ofisi za wakaguzi na kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/15 serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2,064,520,360 kutoka shillingi milioni 335 za mwaka uliopita kwa ajili ya kimarisha shughuli za ukaguzi wa elimu nchini.

- Mh. Kassim Majaliwa pia aliahidi kuwa serikali ina mpango wa kuifanya idara ya Ukaguzi kuwa wakala. Kupitia wizara yake wameamua kuanzisha mamlaka ya Ithibati na Uthibiti katika elimu ngazi ya elimu ya msingi. Ili kuindaa idara ya ukaguzi kuwa mamlaka itaanza kufanya kazi chini ya chombo hicho ili iweze kusimamia shughuli za ukaguzi vizuri.

Je Wajua Hali ya Ukaguzi wa Shule Zetu?

Hali ya ukaguzi bado ni mbaya, uwezo wa serikali kukagua shule hauridhishi. Takwimu zinaonesha kuwa takribani asilimia 19.1% tu ya shule zote za msingi ndizo hukaguliwa kwa mwaka wakati asilimia 21.4 tu ya shule za sekondari ndizo hukaguliwa kwa mwaka. Hii ni kusema takribani asilimia 80% ya shule zote za msingi hazikaguliwi na takribani asilimia 70 ya shule za sekondari hazikaguliwi.

Nishati ya Umeme katika shule za sekondari na msingi

Ahadi ifuatayo ilitolewa na Naibu waziri wa Nishati na Madini Bungeni(29 Mei, 2014) kuhusiana na upatikanaji wa nishati ya umeme shuleni.

- Naibu waziri wa Nishati na Madini Mh. Charles Kitwanga akijibu swali la Mh. Profesa Kuliyokela Kanalwanda Kahigi mbunge wa jimbo la Bukombe, aliyeuliza

ni lini serikali itapeleka umeme katika shule za Msingi na sekondari wilaya ya Bukombe kwani ni kikwazo kikubwa katika ufundishaji na kujifunza mashuleni. Naibu waziri aliahidi kuwa serikali ina mpango wa kupeleka umeme makao makuu ya Bukombe (Ushirombo) pamoja na vijiji/ maeneo ya jirani kupitia mradi wa Electricity "V" ambao ni miongoni mwa miradi iliyopata ufadhili wa benki ya maendeleo ya Afrika AFDB. Mradi huo unahusu kupeleka umeme kwenye vijiji/ maeneo zaidi ya 25 wilayani Bukombe. Mradi utagharimu kiasi cha dola za Marekani 10, 328, 228. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi September 2014 na hivyo kuzinufaisha shule za msingi na sekondari wilayani Bukombe.

Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia

Kwa mujibu wa taarifa za Bunge ahadi zifuatazo zilitolewa na Naibu waziri ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) Mh. Kassim Majaliwa kuhusiana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia mashuleni.

- Mh. Kassim Majaliwa (6 Mei 2014) aliahidi kuwa, serikali imedhamiria kumaliza tatizo la vitabu na madawati shuleni ifikapo mwaka 2016. Katika kufikia azma hii, vitabu vinanunuliwa kwa pamoja (centrally) kupitia fedha za uendeshaji (capitation) zinazotolewa kila mwaka na kuvisambaza mashuleni. Aidha shilingi bilioni 302 zinahitajika ili kufikia uwiano wa kitabu 1 kwa mwanafunzi katika kila somo kwa upande wa shule za msingi, na shilingi bilioni 173 zinahitajika kwa upande wa sekondari ili kila mwanafunzi awe na dawati.

- Serikali itaendelea na juhudi zake za kupunguza uhaba wa madawati nchini. Mh. Majaliwa alieleza

Bunge kuwa zabuni ya utengenezaji wa madawati kutokana na fedha ya chenji ya rada inaendelea na awamu ya kwanza serikali ilitarajia kupata madawati 93,988 na awamu ya pili zabuni imeshatangazwa kwa ajili ya kupata mengine tena. Mh. Majaliwa alisema pia kuwa uhakika ni kwa kila halmashauri katika awamu ya kwanza itapata madawati yasiyopungua 600 na awamu ya pili kila halmashauri itapata madawati yasiyopungua 400).

Ualimu: Uhaba /Maslahi ya walimu

Kwa mujibu wa taarifa za Bunge ahadi zifuatazo zilitolewa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za mikoa na serikali za mitaa: Mh. Kassim Majaliwa (12 Mei, 2014)

- Mh. Majaliwa (12 Mei, 2014) akijibu swali la Mh. Selemani Said Jafo mbunge wa kisarawe lililokua likiuliza Je, ni lini serikali itamaliza tatizo la walimu wilayani Kisarawe;-Alijibu katika ajira mpya ya mwaka 2014 Halmashauri ya wilaya ya Kisarawe imepangiwa walimu 341 wakiwemo walimu wa shule za msingi 178 na walimu wa shule za sekondari 163 na hivyo kutosheleza mahitaji ya walimu 780 wa shule za msingi huku shule za sekondari zikiwa na upungufu wa walimu wa sayansi 82. Kwa hali hii ifikapo mwaka 2017 serikali itamaliza upungufu wa walimu katika halmashauri ya wilaya ya Kisarawe.

- Serikali ina mkakati ambao pia unasimamiwa na wizara ya Elimu kuanzia mwaka huu wa masomo, walimu kuanzia ngazi ya stashahada wenye daraja la kwanza watapatiwa Ruzuku na daraja la pili na la tatu watapatiwa mikopo ili kwenda kusoma masomo ya sayansi. Hii itakuwa motisha kwa walimu wote ambao wataenda kusoma masomo ya sayansi ili kupata idadi ya walimu wengi.

- Serikali itaendelea kulipa malimbikizo mbalimbali ya walimu na mkakati wa serikali ni kuhakikisha kuwa madeni yote yanalip-

wa katika mwaka huu wa fedha 2014/15. Ifikapo mpaka Juni 2014 zoezi la uhakiki wa madeni ya walimu yaliyobaki litakuwa limekamilika na madeni ya upande wa mishahara ambayo yanalipwa moja kwa moja na Hazina yatakuwa yameshalipwa kwa kiasi kikubwa. Mh. Majaliwa alieleza bunge pia kuwa kuwa mpaka kufikia mwezi February 2014, tayari serikali ilikuwa imeshalipa shilingi bilioni 19

Miundombinu ya shule

- Ahadi zifuatazo zilizotolewa na Naibu waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za mikoa na serikali za mitaa: Mh. Kassim Majaliwa Bungeni Mei 12, 2014 Mh. Kassim Majaliwa 12 Mei 2014 akijibu swali lililoulizwa na Mh. Lolesia Jeremiah Bukwimba mbunge wa Busanda aliyetaka kujua serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu katika shule za msingi Nyamsebehi, Mnekezi, Shilabela, Buyaga, Kageye, Ntono na Nyasalala katika jimbo la Budan. Naibu waziri alisema kwa mwaka huu wa fedha 2014/15 serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika halmashauri 40 na kila halmashauri imetengewa shilingi milioni 500. Naibu waziri alieleza pia kuwa: “lakini mpango wa tatu, ni ule ambao sasa Halmashauri zenyewe kupitia mabaraza yao, lazima tumewaagiza kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya shule zilizo pembezoni ili mwalimu anapokwenda aweze kufanya kazi yake vizuri mahali salama” (Kumbukumbu za bunge 19/5/2014).

Elimu ya Ufundi

Kwa mujibu wa taarifa za Bunge ahadi zifuatazo zilitolewa Mei 6, 2014 na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mh. Shukuru Kawambwa akijibu swali la mbunge wa Kagera Mh. Jasson Rweikiza aliyetaka kujua mpango wa serikali kuanzisha chuo cha mkoa cha VETA.

- Mh. Shukuru Kawambwa (6 Mei, 2014)aliahidi kuwa serikali

imetenga fedha itakayowezesha kujenga vyuo 5 vya VETA vya wilaya mwaka 2014/2015. Pia Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mh. Shukuru Kawambwa alieleza bunge kuwa serikali imekopa fedha kutoka African Development Bank ambayo itawezesha kujenga vyuo vya Ufundi vya mikoa minne ambayo ni mipya; Manyara, Geita, Simiyu na Njombe.

- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mh. Jenister mhagama pia alitoa agizo kwa mkurugenzi wa VETA Tanzania kukipandisha hadhi chuo cha VETA Kagera kiwe na hadhi ya chuo cha mkoa.

Hitimisho:

HakiElimu tunashauri mambo makubwa 2 ili ahadi hizi zitekelezwe;

Moja: Wizara ambazo zimeahidi kufanya jambo katika sekta ya elimu zitekeleze ahadi zake. Wizara hizo ni lazima zihakikishe kuwa mipango iliyowekwa inakamilika kwa wakati.

Mbili; Jamii haina budi kufuatilia utekelezaji wa ahadi za serikali ili kuboresha mazingira ya utoaji elimu nchini na kufanikisha zana ya utawala bora na uwajibikaji kwa upande wa serikali.

SL P 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu. (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 215244
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org